JAMHURI YA MUUNGANO WA

TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA TABORA

TABORA



+

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**


**Namba za Simu......................**
**Mkuu wa Shule 0755297005**
**Makamu Mkuu wa Shule Utawala: 0757051769**
**Makamu Mkuu wa Shule Taaluma: 0753671642**

**Shule ya Sekondari TABORA BOYS,**
**S.L.P. 374,**

**Tarehe...............,**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**.................................................**
**S.L.P ...........................................**
**.................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WAVULANA TABORA MANISPAA YA TABORA MKOA TABORA MWAKA............**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka...............na atasoma tahasusi ya...........

Shule ya Sekondari ya **Wavulana Tabora** ipo umbali wa Kilometa 3 kutoka stendi kuu ya mabasi na kilometa mbili 2 kutoka stesheni ya reli. Usafiri wa bajaji au pikipiki kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **TABORA Nauli** ni Shilingi 1500/= kwa pikipiki na Shilingi **3000/=** kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe kama itakavyotangazwa na Serikali anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ....................Mwisho wa kuripoti ni tarehe ........................

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Suruali mbili za kaki (**ESTERN NO 1**) yenye marinda isiwe ya kubana wala mtepesho.
ii. Mashati **mawili (02)** meupe tetron mikono mifupi.(tomato)
iii. Sare ya Michezo ni Bukta nyekundu 02 na Fulana nyekundu 02 zisiwe na maandishi, na viatu vya michezo.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi pea mbili
v. Soksi jozi tano nyeupe.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
vii. Sweta la bluu (v shape)
viii. Nguo za kushindia Suruali 02 nyeusi ya kitambaa yenye marinda mawili isiwe ya kubana mwili au mtepesho *(shamba dress)*.
ix. Tai ya kaki ndefu rangi ya suruali ya kaki ziwe mbili.
x. Tisheti (T-shirt) ya shule nzito, ya kijivu yenye kola nyeusi.
xi. Truck suit ya rangi nyekundu yenye mstari mweupe kwa pembeni.
xii. Trunker la chuma kwa ajili ya kutunzia vitu vyake na kufuli imara.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -

i. Madaftari kauntebook quire4 9 tisa
ii. **Ream (A4)** Mbili (2)
iii. Vitabu vya masomo ya (PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY BASIC APPLIED MATHEMATICS kwa wanafunzi wa PCB), (ADVANCED MATHEMATICS, CHEMISTRY, PHYSICS kwa wanafunzi wa PCM) (HISTORY, GEOGRAPHY, ENGLISH LANGUAGE kwa wanafunzi wa HGL) na GENERAL STUDIES kwa wanafunzi wote. mwandishi (TIE)TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION.
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator pamoja na lab koti nyeupe na gloves kwa tahasusi za sayansi.
vi. Godoro size futi mbili na nusu kwa sita
vii. Mashuka Jozi 2 ya blue na foronya zake pamoja na mto, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua ya blue1 size nne kwa sita, tochi 1 ya betri isiwe ya kuchaji kwenye umeme

viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;dumu la lita tano la kuwekea maji ya kunywa.
xi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, panga moja (1)
xii. mifagio wa ndani wenye mpini mrefu 1 (soft broom.
**xiii.** Mfagio wa nje wenye mpini mrefu(local broom
xiv. Hardbroom yenye mpini mrefu
xv. Kibandizio (squeezer
xvi. Brush imara ya kusugulia chooni(ndani ya sink la choo)
xvii. Nakala ya result slip na nakala ya cheti cha kuzaliwa

**2.3 Michango mbalimbali**

| **Na** | **Aina ya Michango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5000/= |
| 3 | Nembo | 5000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**Shule za Bweni michango hii iwekwe kwenye account namba 51006600072 jina la akaunti TABORA BOYS PROJECT AND PARENTS FUND BENK YA NMB**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. **Ni** marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. iKutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya yote awapo shulen
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

*NB: Hakikisha mtoto anakuja na kadi ya bima ya afya kwa sababu gharama za matibabu ni kubwa sana na zinagharamiwa na mzazi, kama hana kadi ya bima aje na namba ya nida kwa wenye umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea*

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

**FORM NO.1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants.

Pupil's full name

.Age/Years Sex

.Blood found (red and White)

.Stool examination:

.Urinalysis:

.Venereal Diseases test:

.T.B. test:

.Eye Test:

.Ears:

.Chest:

.Spleen:

.Abdomen:

.Urine for Pregnant:

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairrnent(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature: .

Designation: .

Station: Date:

Official Stamp: .

## FOMU NO. 2

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI NA AHADI YA MZAZI KUKUBALIANA NA MASHARTI YA MWANAE KUJIUNGA NA SHULE HII.**

1. Jina la mwanafunzi: ……………………………………………………………………..
2. Tarehe ya kuzaliwa ………………… Mwezi ……………… mwaka …………..…….
3. Amezaliwa katika wilaya: ……………………..….. 4. Uraia …………………………..
4. Shule anakotoka: ………………………………………………………………………
5. Mahali anapoishi kwa sasa: …………………………………………………………….

   Wilaya ……………………………… Tarafa ………………………….
   ,Kata.………………………….., Mtaa/Kijiji ………………………………………..

6. **Dini**: ………………………………………………………………………………
7. Jina la mzazi/rnlezi: ……………………….. ………………………………….
   (a) Anwani ya mzazi/Mlezi: ……………………………… Mabadiliko yawasilishwe ofisini mara moja
   (b) Simu ya (Nyumbani/Mkononi) …………………………………………..……….

8. Unataarifiwa kuwa shule hii ni shule ya Serikali wala siyo ya **DINI** yoyote.
   Aidha inazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu. Hivyo, kila siku ya Ijumaa, Jumamosi na Jumapili wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na Imani zao. Aidha, kumepangiwa vipindi viwili vya dini katika ratiba ya masomo kwa siku ya Ijumaa na kila siku jioni dini baada ya chakula kuanzia saa 1:00 – 1:45 usiku. Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba zingine za shule. **Mzazi amshauri mtoto vizuri kuzingatia agizo hili bila kuleta sababu zozote.**
9. Ahadi ya mwanafunzi: Mimi ……………………………………………………….. ninakubali/Si.kubali kutii kikamilifu kanuni, Sheria na maagizo ya Shule yaliyotolewa hapo, kinyume cha hayo nikufukuzwa shule na ndiyo mwongozo wangu mpaka kumaliza shule.
   Saini ya mwanafunzi: ………………………………………………………….

10. Ahadi ya mzazi/mlezi: ………………………………………………………….
    Nakubali/sikubaliani na maagizo yaliyotolewa hapo juu. Naahidi mwanagu akienda tofauti afukuzwe shule.
    Jina la mzazi/Mlezi: ……………………………… Saini …………… tarehe ……..

| PICHA NA.1 | PICHA NA.2 | PICHA NA.3 | PICHA NA. 4 |
|---|---|---|---|
| No. simu; | No. simu; | No. simu; | No.SIMU |

Zibandikwe picha za wazazi/walezi watakaotambulika shuleni pamoja na namba zao za simu. Mwanafunzi aje na picha mbili (passport size) za kwake na picha nne za walezi (passport size)

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye** ni **mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA** NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA **KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0755297005**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0757051765**
- **Makamu Taaluma 0753671642**
- **Mwalmu wa Afya 0764736088**
- **Mwalimu wa Nidhamu 0620476629**

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SAN SHULE HII**

**DEOGRASIAS A. MWAMBUZI**
**MKUU WA SHULE**

W&UL WA SULE
SHULE YA SEKONDARI TABORA WAVDLANA